# IMAM AL-MEHDI

*Kimeandikwa Na:*
**Hujjatul Islam Wal Muslimeen**
**Al-Haj Sayyid Muhammad Rizvi**

*Kimetolewa Na:*
**BILAL MUSLIM MISSION OF TANZANIA**
**S.L.P. 20033**
**DAR ES SALAAM**

# IMAM AL-MAHDI

Kimeandikwa na:
Hujjatul Islam wal Muslimeen
Sayyid Muhammad Rizvi

Kimetafsiriwa na:
Dr. Muhammad Kanju

Kimechapiswa na:
Bilal Muslim Mission of Tanzania
S.L.P. 20033
Dar es Salaam
Tanzania

Haki za kunakili imehifadhiwa na:
Bilal Muslim Mission of Tanzania

ISBN 9987 620 38 8

Toleo la kwanza: Sha'ban, 1424 / Oktoba, 2003
Idadi: Nakala 2000

Kimetolewa na Kuchapishwa na:
BILAL MUSLIM MISSION OF TANZANIA
S.L.P 20033
DAR ES SALAAM - TANZANIA

# YALIYOMO

Dibaji . . . . . . 1

**Sehemu ya Kwanza**
**Imam wa Kumi na mbili Muhammad Al-Mahdi** . . . . . . 2
1. Kuzaliwa na maisha ya mwanzoni . . . . . . 2
2. Uimam na ghaibu . . . . . . 4
3. Ghaibu ndogo . . . . . . 4
4. Ghaibu kubwa . . . . . . 8
5. Kutokea kwa Al-Mahdi . . . . . . 8

**Sehemu Ya Pili**
**Muongozo katika ghaibu na ujumbe wa Ushia** . . . . . . 10
6. Umuhimu wa kumuamini Al-Mahdi . . . . . . 10
7. Swali la maisha marefu . . . . . . 10
8. Muongozo wa kiroho wa Al-Mahdi (a.s.) . . . . . . 11
9. Ujumbe wa kinafsi wa Kishia . . . . . . 12

# DIBAJI

بسم الله الرحمن الرحيم

الحمد لله ربّ العالمين وأفضل صلوات الله على أشرف الأنبياء
و المرسلين و أكمل تحيّاته على أهل بيته المعصومين و لا سيما بقيّة
الله فى الأرضين و اللّعنة الذائمة على أعدائهم إلى لقاء يوم الدين

Tunamshukuru Allah (s.w.t.) na kwa Baraka za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na Watukufu Ahlul~Bait (a.s.) kwa kutujaalia kuweza kufanikisha juhudi zetu hizi katika kuchapisha kitabu hiki "*Imam Al-Mehdi (a.t.f.).*"

Kitabu kilichopo mikononi mwako ni tafsiri ya moja ya ma'andishi vya Hujjatul Islam wal Muslimeen Sayyid Muhammad Rizvi, na kimetafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili na Dr. Muhammad Said Kanju, kutoka asili yake ya lugha ya Kiingereza.

Bilal Muslim Mission inatoa shukurani zake za dhati kwa wale wote ambao wameshiriki kwa njia moja au nyingine katika kukamilisha kitabu hiki na hivi sasa kipo mikononi mwa wasomaji wetu. Tunamuomba Allah (s.w.t.) awalipe malipo mema hapa Duniani na baadaye huko, Akhera.

و الحمد الله فى الأخرة والا ولى، و صلوات الله على محمّد
وآله هم وسيلة النّجاة، والسّلام على من اتّبع اهدى

**BILAL MUSLIM MISSION OF TANZANIA**
**15, Sha'ban 1424 / 12, Okt 2003**
**Siku ya Kuzaliwa Imam Al-Mehdi (a.t.f.)**

# SEHEMU YA KWANZA

# IMAMU WA KUMI NA MBILI
# IMAM MUHAMMAD AL-MAHDI (A.T.F.)

| | |
|---|---|
| Jina: | Muhammad |
| Kuniya: | Abul Qasim |
| Lakabu: | Al-Mahdi, Al-Qa'im, al-Hujja, Sahib al-Amri |
| Baba: | Hasan bin 'Ali |
| Mama | Narjis (pia anajulikana kama Sausan, Sayqal) |
| Kuzaliwa: | 15 Sha'ban 255 A.H. huko Samarra, Iraq |

Anaishi katika ghayb na atatokea kabla ya mwisho wa wakati

## 1. KUZALIWA NA MAISHA YA MWANZONI

Imam Muhammad al-Mahdi (a.s.) alizaliwa mnamo tarehe 15 Sha'ban 255 A.H. (868 C.E.) huko Samarra na Bibi Narjis, mke wa Imam wa Kumi na Moja Imam Hasan al-'Askari (a.s.). Nasaba ya Bibi Narjis inarejea nyuma mpaka kwa Simon (Sham'un), mmoja wa wanafunzi wa Nabii 'Isa (a.s.); na alikuwa akiheshimiwa sana na Bibi Hakima, dada yake Imam Ali an-Naqi (a.s.) na Kiongozi wa wanawake wa Bani Hashim.

Tangu taarifa juu ya kutazamiwa kuzaliwa kwa Mahdi, yule masihi atakaekomesha dhulma na ukorofi zilipoenea sana, Bani 'Abbas walikuwa wanaiangalia kwa karibu sana familia ya Ahlul Bayt (a.s.). Hali haikuwa tofauti na zile siku kabla ya kuzaliwa Mtume Musa (a.s.) wakati Pharoah (Firauni) alipotoa amri kwamba watoto wote wa kiume wa wana wa Israeli wauawe. Kama vile kuzaliwa kwa Musa kulivyofichwa kwa watu kwa nguvu Zake Allah, kuzaliwa kwa Muhammad al-Mahdi pia kulifichwa kwa watu.

Kwa miaka mitano, Imam al-Mahdi aliishi chini ya malezi ya upendo

ya baba yake. Alikuwa akionwa na watu wa familia tu na wachache waliochaguliwa na baba yake. Hii yote ilifanywa ili kumkinga na wapelelezi wa Bani 'Abbas. Baadhi ya wale waliomuona Imam wakati huo wametajwa hapa chini:

1. Bibi Hakima, shangazi yake Imam Hasan al-'Askari (a.s.)
2. Nasim, mtumishi wa Imam al-'Askari
3. Muhammad bin 'Uthman al-'Amri
4. Husayn bin al-Hasan al-'Alawi
5. Ja'far bin Muhammad bin Malik na kikundi chake
6. Ahmad bin Ishaq

Hapa tutasimulia tu lile tukio ambamo Ahmad bin Ishaq alimuona Imam al-Mahdi. Ahmad, Shia maarufu wa wakati huo, wakati mmoja alimtembelea Imam Hasan al-'Askari (a.s.) na akataka kumuuliza kuhusu mrithi wake. Kabla hata Ahmad hajauliza swali lake, Imam akasema, "Ewe Ahmad! Kutoka siku Alipomuumba Adam, Allah hajaiacha ardhi bila ya mwakilishi (Hujjat au Hoja), wala hataiacha bila muwakilishi mpaka siku ya hukumu. Ni kwa sababu ya Hoja hiyo kwamba Allah anaikinga adhabu kwa watu, ananyeshesha mvua na kuotesha baraka kutoka ardhini".

Ahmad: "Ewe mtoto wa Mtume! Ni nani mrithi na Imam baada yako?".

Imam Hasan al-'Askari mara moja akaingia ndani ya nyumba na akarudi na kijana wa miaka mitatu mikononi mwake, "Ewe Ahmad bin Ishaq, kama hungekuwa mwenye heshma mbele ya Allah na wawakilishi wake, nisingemuonyesha kijana wangu huyu kwako. Jina lake na Kuniya yake ni sawasawa na ile ya Mtume; huyu ndie ambae ataijaza dunia na haki na usawa kama vile tu itakavyokuwa imejazwa na dhulma na ukorofi.

"Ewe Ahmad, mfano wake ni ule wa Khidhr na Dhul Qarnain (ambao wanaaminiwa na Waislam kuwa bado wanaishi.). Wallahi, ataingia kwenye ghayb katika hali ambayo hakuna atakaepata wokovu ila yule ambae Allah atambariki na imani juu ya Uimam wake…."

## 2. UIMAM NA GHAIBU

Baada ya kuuawa shahidi kwa Imam Hasan al-Askari mwaka 260 A.H. Uimam wa Imam Muhammad al-Mahdi (Allah afanye wepesi kutokeza kwake) ukaanza. Uimam wake umegawanyika sehemu mbili:

1. Miaka 69 ya mwanzo kinachojulikana kama kipindi cha "al-Ghaybat 's-Sughra – yaani Ghaibu Ndogo".
2. Kipindi baada ya 329 A.H. kinachojulikana kama "al-Ghaybatu 'l-Kubra – Ghaibu Kubwa."

Uimam wa Imam al-Mahdi (a.s.) ulianza na ghaibu ambayo imeendelea mpaka wakati huu wa sasa. Hata hivyo, wakati wa miaka 69 ya mwanzo, Mashia walikuwa wakipata mawasiliano na Imam kupitia kwa mawakala maalum tu walioteuliwa; ambapo baada ya 329 A.H., hakukuwa na mawakala kama hao walioteuliwa. Ili kuelezea tofauti katika ukweli wa Ghaibu yenyewe, kipindi cha awali kinaelezwa kama "ndogo, pungufu – sughra au qasira", ambapo hiki cha pili kinaelezwa kama "kubwa, kuu-kubra au tawila".

Kama Ghaibu hii ingechukua hali ya kipindi chake "Kikubwa" kutoka siku ile ya kwanza, jumuiya ya Mashia isingeweza kujiweka sawa na hali hiyo kirahisi; kungeweza kuwa na ghasia kubwa na machafuko. Kukua kwa pole pole kwa Ghaibu kumewafanya Mashia kuzoea ile fikra ya kutokuhusiana na Imam moja kwa moja.[1]

## 3. GHAIBU NDOGO

Wakati wa Ghaibu Ndogo, Imam al-Mahdi (a.s.) aliteua wawakilishi wanne maalum, mmoja baada ya mwingine, kama kiungo kati yake na Mashia wake. Kwa kweli, kulikuwa na wawakilishi wengine lakini wenye ukomo wa hukumu au shughuli zenye ukomo.

1 Kwa maelezo haya ya Ghaibu fupi na ndefu, tazama utangulizi wa Allamah Sayyid Saeed Akhtar Rizvi kwa Ibn Shadhan, '*The Return of al-Mahdi*' iliochapishwa Dar es Salaam, London na Bombay.

Mawakala maalum wanne walikuwa kama ifuatavyo:-

1. 'Uthman bin Sa'id al-Amri, aliyejulikana kama Abu Amr.
2. Muhammad bin 'Uthman bin Sa'id, aliyejulikana kama Abu Ja'far.
3. Husayn bin Rawh an-Nawbakhti, aliyejulikana kama Abul Qasim.
4. 'Ali bin Muhammad Samary, aliyejulikana kama Abul Hasan.

'Uthman bin Sa'id alikuwa pia ni Sahaba mashuhuri na wakala wa Imam an-Naqi (a.s.) na Imam Hasan al-Askari (a.s.); alikuwa mwenyeji wa Samarra. Ili kuficha ukiungo wake na kazi pamoja na Imam Hasan al-'Askari kwa watoa habari (informers) wa serikali, 'Uthman bin Sa'id alibadili kazi yake – akawa mchuuzi akiuza mafuta ya kupikia kwenye mkokoteni. Wakati ulinzi mkali wa serikali juu ya nyumba ya Imam ulifanya hali karibu ya kutowezekana kwa Mashia kumtembelea Imam kwa uhuru, 'Uthman huweka barua na masuala ya dini kutoka kwa Mashia katika vyombo vya kuwekea mafuta na kuzifikia nyumbani kwa Imam kwa kisingizio cha kupeleka mafuta ya kupikia!

Ahmad bin Ishaq anasimulia kwamba Imam al-'Askari (a.s.) alimuambia kuwa 'Uthman bin Sa'id alikuwa "Muaminifu, na wakutegemewa katika macho ya Imam aliyepita na mimi mwenyewe pia katika uhai wangu na baada ya kufa kwangu. Chochote atakachokuambia kinatoka kwangu, na chochote atakacholeta kwako kinatoka kwangu."

Wakati 'Uthman bin Sa'id alipokufa, Imam al-Mahdi (a.s.) aliandika barua ya rambirambi kwa mwanae, Muhammad bin 'Uthman, kama ifuatavyo:- "Sisi wote ni wa Allah, na kwake sote tutarejea. Baba yako ameishi maisha ya uadilifu na amekufa kama mtu anaeheshimiwa. Mwenyezi Mungu amshushie Rehma Zake na Amuunganishe na Mabwana Zake. Alikuwa katika kazi yake kwa ajili ya Mabwana Zake, na alifanya bidii katika yaliyompendeza Mungu Mwenye nguvu na Maimam. Allah ampe neema Zake na Amsamehe makosa yake."

Muhammad bin 'Uthman alikuwa ndiye wakala maalum wa pili wa wakati wa Ghaibu Ndogo. 'Abdullah bin Ja'far al-Himyari anasema kwamba alipokufa 'Uthman, tulipokea barua toka kwa Imam, katika mwandiko ule ule ambao tuliutambua kutoka kwenye mawasiliano

yaliyopita, ikieleza kwamba Muhammad bin ‘Uthman ameteuliwa katika nafasi ya marehemu baba yake kama wakala maalum mpya wa Imam.

‘Abdullah bin Ja’far wakati mmoja alimuuliza Muhammad bin ‘Uthman, “Umemuona Bwana wa walimwengu (*sahib al-amr*)?” Alijibu, “Ndio, mkutano wangu na yeye wa mwisho ulikuwa karibu na Nyumba tukufu ya Allah (yaani Ka’bah) ambapo nilimsikia akiomba, “Ewe Allah nitimizie mimi kile ulichoniahidi ….”

Muhammad bin ‘Uthman pia amesema kuwa Imam al-Mahdi (a.s.) anakuwepo kila mwaka katika matendo ya hijja, anawaona watu na kuwatambua, na wao pia wanamuona lakini hawamtambui.

Husayn bin Rawh alikuwa ndiye wakala maalum wa Imam. Aliheshimiwa sana na Waislam wote; alifanya kazi kwa karibu sana na ‘Uthman bin Sa’id.

Siku chache kabla ya kifo chake, Muhammad bin ‘Uthman alikuwa amemfahamisha Husayn bin Rawh kwa wazee wa jumuiya ya Mashia kama wakala maalum wa Imam, atakayefuata. Ja’far bin Ahmad Qummi alikuwa ndiye mtu wa karibu sana na masahaba wote wa Muhammad bin ‘Uthman, na Mashia wengi walidhani kwamba atamfuatia Muhammad kama wakala maalum mwingine. Wakati wa kifo cha Muhammad, Ja’far alikuwa amekaa karibu na kichwa cha kitanda ambapo Husayn bin Rawh alikuwa amekaa miguuni kwake. (Katika mashindano hayo ya kitamaduni, kukaa kichwani ilikuwa ni nafasi ya heshima zaidi.) Muhammad bin ‘Uthman aligeuza kichwa chake kumuelekea Ja’far na akasema, “Nimeamriwa kukabidhi masuala yote kwa Abul Qasim Husayn bin Rawh.” Wakati Ja’far aliposikia hili, alisimama, akaenda kwa Husayn, akamshika mkono wake na akamfanya akae karibu na kichwa cha kitanda ambapo yeye mwenyewe akakaa miguuni kwa Muhammad.

Katika barua iliyoandikwa tarehe 6 Shawwal 305, Imam al-Mahdi (a.s.) aliandika kuhusu Husayn bin Rawh: “Tunamfahamu; Allah amfahamishe na yote yale ambayo ni bora kwake, na Yeye amsaidie. Tuna habari na barua yake, na tuna matumaini na imani kwake. Anacheo machoni petu ambacho kinamridhisha; na Allah ampe ziada katika rehma zake juu yake kwani Yeye hakika ndiye Bwana na Ana nguvu juu ya kila kitu. Sifa zote

ni zake Allah ambae Hana mshirika na Rehma na Amani Zake Allah ziwe juu ya Mtume Wake, Muhammad, na Kizazi chake."

Wakati Abu Sahl an-Nawbakhti, mtafiti maarufu wa kidini wa Kishia wa wakati ule, alipoulizwa ni kwa nini amepitwa na Husayn bin Rawh katika kuchukua cheo cha wakala maalum wa Imam, alijibu: "Wao (i.e. Maimam) wanajua zaidi ni nani awezaye kuwawakilisha wao. Mimi ni mtu ambae ninahojiana dhidi ya mpinzani wangu na hasira. Kama ningekuwa ndiye msaidizi maalum wa Imam na nikawa nimejua alipo Imam – kama ambavyo Husayn bin Rawh anajua ningeweza kupataje katika msisimko wa mahojiano (kama nikibanwa kutaja alipo Imam). Lakini Abul Qasim (Husayn bin Rawh) yu kama vile kama Imam angekuwa amejificha chini ya joho lake, asingelinyanyua hata kama alikuwa akatwe vipande vipande kwa visu vikali."

Husayn bin Rawh alitumika katika cheo hiki kwa miaka 21 mpaka kifo chake mwaka 326 A.H. huko Baghdad.

'Ali bin Muhammad as-Samary alikuwa msaidizi maalum wa nne wa Imam. Usaidizi wake ulikuwa kwa ulinganisho ni mfupi sana. Alikufa mwaka 329 A.H. Kabla ya kifo chake, wakati baadhi ya Mashia mashuhuri walipouliza juu ya msaidizi maalum anaefuata, alijibu, "Sikuamrishwa kuteua yeyote baada yangu."

Siku sita kabla ya kifo cha as-Samary, alipokea barua ifuatayo kutoka kwa Imam al-Mahdi (a.s.):
"Ewe 'Ali bin Muhammad as-Samary. Allah awatawalie jamaa zake katika kuadhimisha huzuni juu yako. Utaiacha dunia hii baada ya siku sita. Kamilisha shughuli zako na usimteue yeyote kama mrithi wako. Hakika, ile Ghaibu kubwa imeanza. Hakutakuwa na kujitokeza kwangu mpaka Allah mwenye uwezo aniamrishe mimi; na hiyo itakuwa baada ya muda mrefu, baada ya mioyo imekuwa migumu na dunia imejaa dhuluma.
Muda mfupi tu, baadhi ya watu watadai kuwa wameniona (na kudai cheo cha usaidizi maalum). Tahadhari kwamba atayefanya madai kama hayo kabla ya kutokeza Sufyani na Sayha ni muongo na mdanganyifu. Na hakuna uwezo na nguvu ila kwa Allah. Aliye juu, Mkubwa."

## 4. GHAIBU KUBWA

Kinyume na Ghaibu Ndogo ambapo Mashia waliweza kuwasiliana na Imam wao kupitia kwa wasaidizi maalum, katika Ghaibu kubwa, hakuna msaidizi maalum. Imam al-Mahdi (a.s.) atatokeza kutoka kwenye Ghaibu wakati wowote Allah akiruhusu yeye kufanya hivyo ili kuweka utawala wa Mungu duniani na kufuata dhulma na ukorofi mara moja na kudumu.

Wakati wa Ghaibu kubwa, wale Mashia ambao hawana ujuzi wa kuzifikia sheria toka kwenye Qur'ani na sunna za wale 'wasiokosea' wafuate maelekezo yanayotolewa na wale wajuzi. Mtu anaejulikana kama Ishaq bin 'Ammar aliuliza katika barua kwa Imam al-Mahdi (a.s.) kuhusu muongozo wakati wa Ghaibu Kubwa. Imam mtukufu aliandika: "Na kwa yale matatizo mapya yanayojitokeza (ambayo hayakutajwa katika Qur'ani na Sunna), rejeeni kwa wale wanaosimulia hadithi zetu [Maulama'a] kwa vile wao ni hoja zangu juu yenu kama nilivyo hoja ya Allah juu yao."

## 5. KUTOKEA KWA AL-MAHDI

Kama ilivyotajwa hapo juu, hata Imam al-Mahdi (a.s.) mwenyewe anangojea rukhsa ya Allah kwa kutokeza kwake. Hii ina maana kwamba hakuna mtu anayejua huo wakati wa kutokeza Imam. Tunazo hadithi za wazi zinazosema kwamba wale wanaoongea kuhusu wakati ambapo Imam atafanya kujitokeza kwake ni wa kuitwa waongo. Katika barua iliyotajwa mapema, Imam al-Mahdi (a.s.) ameandika, "Na kwa kutokeza kwa wokovu (kwa mimi), kutajwa kwake kuna Allah Mwenye nguvu zote na wale wanaouweka wakati ni waongo."

Hata hivyo, kuna hadithi nyingi zinazoelezea zile dalili kabla ya kutokeza kwa Imam al-Mahdi (a.s.). Baadhi ya alama hizi ni kama zifuatazo:-

1. Dhuluma, ukorofi na matendo ya dhambi yatakuwa ya kawaida ulimwenguni kote.

2. Kutokeza kwa Sufyani na kuvunjwa kwa jeshi lake. Sufyani ameelezwa kama Msyria kwa jina la 'Uthman bin 'Anbasa kutoka kwenye kizazi cha Yazid bin Muawiyah.

3. Maasi yatatokea ya mtu aitwae Hasani Sayyid huko Iran. Ataunda serikali ya haki ya Kiislamu na kuwaita watu kwenye Uislam. Atakuwa huko Kufa wakati habari za kutokeza kwa Imam al-Mahdi (a.s.) huko Makka zitaenea dunia nzima. Huyo Hasani Sayyid atakuja Makka na kutoa kiapo cha utii kwa Imam al-Mahdi (a.s.)

4. Mara baada ya kutokeza kwa Imam al-Mahdi huko Makka, sauti ya kimbinguni itasikika duniani pote ambayo itamtambulisha Imam al-Mahdi kwa watu wote.

5. Kushuka kwa Nabii ʻIsa (a.s.) kutoka mbinguni kwenye mji wa Damascus. Atasali nyuma ya Imam al-Mahdi.

Baada ya Ghaibu ndefu sana, kwa amri ya Allah, Imam al-Mahdi (a.s.) atafanya kujitokeza kwake kujulikane ndani ya Msikiti Mtukufu huko Makka na kuanza ujumbe wake wa kuanzisha utawala wa Allah katika ardhi.

Watu mia tatu na kumi na tatu watatoa kiapo cha utii kwake, na halafu ataondoka kuelekea Madina. Kutoka Madina, al-Mahdi ataelekea Kufa, Iraq. Baada ya hapo Nabii ʻIsa atashuka huko Damascus na kujiunga na Imam al-Mahdi (a.s.)

Makao Makuu ya Imam al-Mahdi yatakuwa Kufa ambapo atatawala ulimwengu mzima. Wakati wa utawala wa Imam, rehma za Allah zitakuwa tele; hakutakuwa na umaskini; amani na usalama vitakuwa ndio sheria ya siku.

Ewe Allah, teremsha Rehma zako juu ya Mtume Muhammad na Kizazi chake.
Ewe Allah, kuwa Bwana, Mlinzi, Kiongozi na Jicho
Kwa Muwakilishi wako, Hoja,
mtoto wa Imam Hasan al-ʻAskari,
Katika saa hii, na katika kila saa mpaka,
Unamuimarisha juu ya ardhi kwa muda mrefu.

# SEHEMU YA PILI

# MUONGOZO KATIKA GHAIBU NA UJUMBE WA USHIA

## 1. UMUHIMU WA KUMUAMINI AL-MAHDI

Ghaibu ya Imam ni wakati wa mtihani kwa Waumini. Lakini imani kwa Imam al-Mahdi ni wa lazima sana kwa ukombozi. Imam Hasan al-'Askari (a.s.) alisema, "Ninaona kwamba baada yangu tofauti zitatokea miongoni mwenu kuhusu Imam wa baada yangu. Yeyote atakayekubali Maimam baada ya Mtume wa Allah lakini akamkataa mwanangu ni kama mtu anayewakubali Mitume wote lakini akaukataa utume wa Muhammad, Mtume wa Mungu, juu yake ambaye amani na rehma. Na yeyote anaemkataa (Muhammad) Mtume wa Allah ni kama mtu ambaye amewakataa Mitume wote wa Allah, kwani kumtii wa mwisho katika sisi ni kama kumtii wa kwanza na kumkataa wa mwisho katika sisi ni kama kumkataa wa kwanza. Lakini tahadhari! Hakika kwa mwanangu kuna Ghaibu, wakati ambamo watu wote wataangukia kwenye shaka isipokuwa wale ambao Allah anawalinda."

## 2. SWALI LA MAISHA MAREFU

Wapinzani wa Ushia wanapinga kuwa kulingana Imani za madh-habi hiyo huyo Imam Aliyefichwa atakuwa mpaka sasa ana umri wa karne kumi na mbili, ambapo hii haiwezekani kwa binadamu yeyote.

Katika jibu ni lazima isemwe kwamba kupinga huku kumeegemea tu katika kutokuwezekana kwa kutokeza kama huko, sio ugumu wake. Kwa kweli muda mrefu wa kuishi kama huo au maisha ya kipindi kirefu sana hayawezekani. Lakini wale wanaosoma hadithi za Mtume Mtukufu na Maimam wataona kwamba zinarejea kwenye maisha haya kama mtu mwenye sifa za miujiza. Miujiza bila shaka sio haiwezekani wala haiwezi

kukanushwa kwa hoja za kisayansi. Haiwezekani kamwe kuhakikishwa kwamba viasili na nguvu zao vinavyofanya kazi katika dunia hii ni vile tu tunavyoona na kufahamu na kwamba viasili vingine tusivyofahamu au ambavyo athari zake na matendo yake hatujayaona wala kuyafahamu hayajakuwepo. Ni kwa njia hii inayowezekana kabisa kwamba katika mmoja au wengi katika jamii ya wanadamu kunaweza kukafanya kazi baadhi ya viasili na nguvu zao ambavyo vinaweka juu yao maisha marefu sana ya miaka elfu moja au maelfu ya miaka. Utabibu wala haujapoteza tamaa ya kugundua njia ya kuweza kupata mzunguko mrefu sana (life span) wa maisha. Katika hali yoyote, kukataa huku kwako kwa "watu kitabu" kama Wayahudi, Wakristo na Waislam ni kwa ajabu sana kwani wanaikubali miujiza ya Mitume wa Mungu kulingana na maandiko matakatifu yao wenyewe.

## 3. MUONGOZO WA KIROHO WA AL-MAHDI (A.S.)

Wapinzani wa Ushia vile vile wanapinga kwamba, ingawa Mashia wanamchukulia Imam kwamba ni muhimu ili kueleza sheria za dini ili kuwaongoza watu, hii Ghaibu ya Imam ndio mkanusho wa kusudio hili hasa, kwani Imam aliyeko Ghaibu ambae hawezi kufikiwa na watu hawezi kuwa kwa njia yoyote ile ni mwenye kunufaisha au mwenye kuileta athari. Wapinzani hao wanasema kwamba kama Mungu angependa kuleta Imam kuwaongoza watu ana uwezo wa kumuumba katika muda unaohitajika wala hahitaji kumuumba maelfu ya miaka kabla.

Katika jibu ni lazima isemwe kwamba watu kama hao hawajaelewa hasa maana ya Imam huyu kwani kazi za Imam sio tu ule utaratibu wa kuelezea elimu za kidini na muongozo wa wazi kwa watu. Katika njia ile ile kwamba ana jukumu la kuongoza watu kwa nje, Imam pia anathibitisha kazi za wilayah (uongozi) na muongozo wa wazi kwa watu. Ni yeye anamuelekeza mwanadamu katika maisha yake ya kiroho na kuiongoza hali ya ndani ya vitendo vya mwanadamu kumuelekea Allah. Ni dhahiri, kuweko kwake kimwili au kutokwepo kwake hakuna uzito katika suala hili. Imam anawaangalia watu kwa ndani na yuko kwenye ushirika na roho na nafsi za watu hata kama amefichika kutoka kwenye

macho yao halisi. Kuishi kwake, daima ni muhimu hata kama wakati wake haujafikia wa kudhihiri kwake kwa nje ujenzi upya wa ulimwengu ambao anapaswa kufanya.

## 4. UJUMBE WA KINAFSI WA KISHIA

Ujumbe wa Ushia kwa ulimwengu unaweza kufanyiwa mukhtasari kwa msitari mmoja: "Kumjua Allah". Au kwa maneno mengine, ni kumuamrisha mwanadamu kufuata njia ya ufunuo mtakatifu na elimu ya Mungu ili kupata ustawi na wokovu. Na ujumbe huu umo kwenye aya ile ile ambayo kwayo Mtume alianzia kazi yake ya utume aliposema, "Enyi watu! Mjueni Mwenyezi Mungu katika umoja wake (na kumtambua Yeye) ili kwamba mpate wokovu."

Kama mukhtasari wa malezo ya ujumbe huu tutaongeza kwamba mwanadamu ameambatana na maumbile kwa malengo mengi katika maisha haya ya kidunia na anasa za mapambo yake. Anapenda vyakula vyenye ladha na vinjywaji, mavazi ya mitindo, majumba ya kuvutia na mazingira yake, mke mzuri mwenye kupendeza, marafiki waaminifu na utajiri mkubwa. Na katika muelekeo mwingine anavutwa na mamlaka ya kisiasa, cheo, umaarufu, kupanuka kwa utawala na milki yake na kuvunjwa kwa chochote kinachopingana na mapenzi yake.

Lakini katika hali yake ya ndani na ustawi wa akili ya asili mwanadamu anaelewa kwamba haya yote ni mahitaji yaliyoumbwa kwa ajili ya mwanadamu, lakini mwanadamu hakuumbwa kwa ajili ya hayo. Vitu hivi vinatakiwa viwe na utii kwa mwanadamu na vimfuate sio kinyume chake. Kudhania tumbo na eneo lililo chini yake kama jambo la mwisho katika maisha ni fikra za ng'ombe na kondoo. Kuchana, kukata na kuangamiza wengine ni fikra za chui mkubwa (Tiger), mbweha na mbwa mwitu.

Fikra ya asili katika maisha ya mwanadamu ni kule kupata maarifa na sio kinginecho. Fikra hii iliyojengeka juu ya maarifa (pamoja na nguvu iliyonayo kupambanua baina ya kweli na uongo), inatuongoza sisi

kuelekea kwenye ukweli na sio kuelekea kwenye mambo ambayo maoni yetu yanayotaka au kuelekea kwenye tamaa, uroho na ubinafsi. Fikra hii inamuangalia mwanadamu kama sehemu ya ukamilisho wa kuumbwa bila uhuru uliojitenga au uwezekano wa kujipenda kwenye uasi. Kinyume na imani iliyopo kwamba mwanadamu ndiye mdhibiti wa maumbile na anafuga asili yenye maasi na kuishinda ili itii mapenzi na matamanio yake, tunaona kwamba mwanadamu mwenyewe kiukweli ni chombo katika asili ya ulimwengu na anatawaliwa na kuamriwa nayo.

Fikra hii iliyojengeka katika misingi ya maarifa inamkaribisha mwanadamu kutafakari kwa karibu zaidi juu ya ufahamu alionao wa kuwepo kwa dunia hii mpaka iwe wazi kwake kwamba hii dunia ya kuishi na vyote vilivyomo haikujiweka yenyewe lakini zaidi kutokana na chanzo kisicho na mwisho. Ndipo tena atajua kwamba uzuri wote na ubaya wote, viumbe vyote hivi vya duniani na angani, vinavyoonekana kama ukweli wa wazi unaojitegemea, vinapata kuwa kweli tu kwa kupitia ukweli mwingine na vinadhihirishwa tu katika nuru yake, sio kwa vyenyewe au kupitia vivyo vyenyewe. Katika njia hiyo hiyo ambayo "ukweli" na vilevile nguvu na utukufu wa jana havina thamani kubwa kuliko hadithi na visa vya leo, vivyo kwa ukweli wa leo sio zaidi kama ukweli wa kesho.

Katika uchambuzi wa mwisho, kila kitu, chenyewe, sio zaidi ya hadithi na ndoto. Ni Allah peke yake aliye wa kweli katika fahamu yote, Yeye asiyefutika. Chini ya ulinzi wake, kila kitu kinapata kuishi na kinadhihirika kupitia Nuru ya Asili Yake. Kama mtu anajaaliwa na uono na nguvu ya fahamu, basi hema lake la kuwepo kwake kwa kujitenga litaanguka mbele ya macho yake kama tone la povu (Bubble) juu ya usawa wa maji. Ataona kwa macho yake kwamba dunia na vyote vilivyomo vinategemea juu ya mtu asiye na Mwisho, ambae ana maisha, uwezo, maarifa na kila ukamilifu kwa kiwango kisicho na mwisho. Mwanadamu na viumbe vingine vyote katika dunia ni kama madirisha mengi ambayo yanafanya maonyesho kulingana na uwezo wao dunia isiyo na mwisho ambayo inawapatia mbali na kulalia upande mwingine kabisa nao.

Ni katika muda huu ambapo mwanadamu anapata kutoka kwake na

kwa viumbe wengine ule ubora wa uhuru na ubora na kuzirudisha sifa hizi kwa Mwenyewe. Anajiondoa yeye mwenyewe toka kwenye vitu vyote na kujifungamanisha mwenyewe moja kwa moja kwa Mungu Mmoja. Mbele ya Enzi Yake na Utukufu hafanyi chochote ila kuinama kwa unyenyekevu. Hapo ndipo tu anapokuwa ameongozwa na kuelekezwa na Allah ili kwamba chochote atakachojua anakijua katika Allah. Kupitia muongozo mtukufu anakuwa amepambwa na uadilifu na fadhila za kiroho na vitendo halisi ambavyo ni sawa na Uislam wenyewe, utii kwa Allah, dini ambayo iko katika ukamilifu wa asili wa vitu.

Hili ni daraja la juu la ukamilifu wa mwanadamu na hali ya mtu mkamilifu (*insanu 'l-kamil*), yaani Imam ambaye amefikia cheo hiki kwa baraka za Mungu. Juu ya hayo, wale ambao wamefikia hali hii kwa ibada ya njia za kiroho, na vyeo tofauti na hali walizonazo, ndio wafuasi wa kweli wa Imam. Inakuwa wazi kwa hiyo kwamba elimu ya Mungu na ya Imam haitofautiani (yaani elimu ya Imam ni ile itokayo kwa Mungu) katika njia hiyo hiyo ambayo elimu ya Mungu imeunganishwa bila kufunguliwa na elimu ya (Imam) mwenyewe. Kwani yeyote anayejua mfano wa kuwepo yeye mwenyewe atakuwa amekwishajua ukweli wa kuwepo ambako ni kwa Mungu pekee ambaye yu mwenye kujitosheleza na bila ya kuhitaji kitu chochote kile kiwacho.

**MWENYEZI MUNGU ANASEMA:**

يَوْمَ نَدْعُو كُلَّ أُنَاسٍ بِإِمَامِهِمْ ۖ فَمَنْ أُوتِيَ كِتَابَهُ بِيَمِينِهِ فَأُولَـٰئِكَ يَقْرَءُونَ كِتَابَهُمْ وَلَا يُظْلَمُونَ فَتِيلًا ﴿٧١﴾

(Ewe mwanadamu! Ikumbuke) siku Tutakapowaita kila watu pamoja na Imamu wao; basi atakayepewa kitabu (chake cha Amali) kwa mkono wa kulia, hao watavisoma vitabu vyao (kwa furaha); ...

(Bani Isra'il, 17:71)

**MTUKUFU MTUME (S.A.W.W.) AMESEMA:**

من مات و لم يعرف إمام زمانه، مات ميتة جاهلية

"Yeyote yule afaye pasi na kumjua Imamu wa zama zake, atakuwa kafa kifo cha ujinga".

**MTUKUFU MTUME (S.A.W.W.) AMESEMA:**

"Hao (Ulul Amr watajwao mwenye Qur'ani 4:59) ni Makhalifa wangu na Maimamu wa Waislamu baada yangu. Wa kwanza ni Ali, kisha ni Hassan, kisha ni Husayn, kisha ni Ali bin Husayn, kisha ni Muhammad bin Ali, kisha ni Jafar bin Muhammad, kisha ni Musa bin Jafar, kisha ni Ali bin Musa, kisha ni Muhammad bin Ali, kisha ni Ali bin Muhammad, kisha ni Hassan bin Ali, kisha ni Muhammad bin Hassan (Mahdi)..".

("Kifayatul Athar" na rawdhatul ahbab, vya Hafidh Jamaluddin Muhaddith).

**MTUKUFU MTUME (S.A.W.W.) AMESEMA:**

(Ewe Husain), wewe u Sayyid, mwana wa Sayyid, na ndugu wa Sayyid; wewe tu u uthibitisho (wa Mwenyezi Mungu) mwana wa uthibitisho (wa Mwenyezi Mungu) na ndugu wa uthibitisho (wa Mwenyezi Mungu); na baba wa uthibitisho tisa ambao wa tisa wao ni Qaim wao ambaye atakuwa al-Mahdi.

**IMAMU HUSAIN AMESEMA:**

"Dhuria wangu wa tisa ni Imam yule atakayeitetea Haki na Mwenyezi Mungu ataihuisha hii Dunia iliyokufa na kwaye dini ya haki itazishinda dini zote. Muda wake wa ughaibu utakuwa mrefu na katika muda huo watu wengi watapotoka na wachache tu watabaki katika imani nao watateswa. Kwani, watu watawaambia, "Kama ninyi ni wakweli, basi tuambieni lini ubashiri huo utatimia". Watavumilia (hao wenye kuamini) na watapata baraka sawa na zile za waliopigana pamoja na Mtume".

ISBN: 9987 620 38 8

Kimechapishwa na Kimetolewa na:
Bilal Muslim Mission of Tanzania
S.L.P 20033
Dar es Salaam